SOMO LA 10

MAFUNZO YA BIBLIA KUHUSU UZIMA WA MILELE (Sehemu ya I)

“Saa yaja ambayo watu wote waliomo makaburini watasikia sauti yake, Nao watatoka; wale waliofanya mema kwa ufufuo wa uzima, na wale waliotenda mabaya kwa ufufuo wa hukumu.” (Yohana 5:28 - 29)

KUSUDI LA SOMO HILI ni kuchunguza yaliyomo katika Biblia ili tujue inasema nini kuhusu uzima wa milele kwa mwanadamu. Kwa sasa tumepitia masomo namba 7,8 na 9 na tumeona ya kuwa hakuna popote ambapo inaeleza tuna uzima wa milele kwa sasa; na wala haitupi sababu zozote za kuonyesha tukifa hatujafa ila tunapita na kwendea maisha mengine. Somo hili litaendeleza na kutilia mkazo dhana hii na kuongezea kulenga inayosema Biblia kuhusu uzima wa milele na sisi; tuutarajie lini, tufanye nini ili tuupate.

Tangu jadi watu wamekuwa wakitamani kuwa na hali ya kutopata uharibifu na hilo lawafanya wajihisi wana uzima wa milele. Hata hivyo, yathibitisha mambo kinyume kabisa; mtu hana uzima wa milele. Mtu kuwa na njaa na kutamani chakula sana haithibitishi kuwa ana chakula. Mtu yeyote anaweza kuona ukweli wa mambo hapa. Ni sawa pia na suala la uzima wa milele. Kama ilivyo ya kwamba mtu akikosa chakula, mtu hufa baada ya muda mfupi, ndivyo ilivyo na uzima wa milele, mtu hufa na kurudia mavumbi ya ardhi.

Katika maandiko mwanadamu anarejelewa kila mara kama mtu wa kufa,na ana maisha mafupi, ya kuangamia: sio wa kudumu na kutoharibika kamwe, au kuwa na maneno yenye mawazo hayo. “Mortality” inatokana na neno la kilatini “Mors” (Kifo), na yamaanisha “hali ya kufa” Chochote ambacho ni “mortal” kwa hivyo hakina budi kife, uwezo wake wa kuishi una kikomo, kwa sababu ya kuwa hali ya kuharibika na kufutika tuliyorithishwa.

Roho wa Mungu ni nguvu ya uzima inayomwekea mtu, na haiwezi kuangamia – na hivyo si kusema ni thibitisho kwa mtu mwenyewe anadumu milele, au ana “cheche ya uzima wa milele” ndani yake. Ingekuwa hivyo, ingethibitisha kudumu milele kwa wanyama, maana wao pia ni “viumbe hai”: kama vile mtu alivyo, akiendelezwa maishani na hii nguvu ya kutia maisha. Roho hii ya nguvu ya uzima ni ya Mungu, na yeye ndiye anayeithibiti, anapeana na kuondoa.

Wanadamu na wanyama wote ni “viumbe hai” sawa, Mungu ameeleza:

“Kwa maana linalowatukia wanyama, jambo moja linawatukia, anavyokufa huyu ndivyo anavyokufa huyu; naam, WOTE WANAYO PUMZI MOJA; (ruach, spirit) wala mwanadamu hana kitu cha kumpita mnyama (katika hali hii) (Mhubiri 3:19).

Musa pia alielezea ukweli huu wa kimsingi; akizungumzia gharika: -

“Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwanadamu, kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa” (Mwanzo 7: 21 - 22)

Hapa tena, watu na wanyama wanaunganishwa pamoja katika kanuni ya uzima. Wote pumzi moja, “pumzi ya uhai” wao (yaani, “pumzi ya roho ya uhai”: neshamah ruach chay).

Ayubu yule mtu mwenye haki anasema:

“Na roho (ruach, pumzi) ya Mungu i katika pua yangu” (Ayubu 27:3).

“Mwacheni mwanadamu ambaye pumzi (neshamah) yake i katika mianzi ya pua yake” (Isaya 2:22)

“Kama (Mungu) akimwekea mtu moyo wake, akijikusanyia roho (ruach)yake na pumzi (neshamah) zake, wenye mwili WOTE wataangamia pamoja, nao wanadamu watarejea tena kuwa mavumbi” (Ayubu 34:14)

Anagalia kwa makini ni roho wa Mungu. Mwanadamu kama alivyo mnyama, anategemea ni kiumbe anayepokea; anamiliki kwa muda tu hizi nguvu zinazompa uhai kutoka kwa Mungu. Inavyosemwa juu ya mwanadamu, ndivyo mtunga Zaburi anavyosema kuwahusu wanyama (104 : 29 - 30)

“Waiondoa pumzi (ruach) yao, wanakufa na kuyarudia mavumbi yao. Waipelekea roho (‘ruach’) yako, wanaumbwa.”

Ilipelekwa wakati wa uumbaji wa viumbe vyote ili vipate kuwa hai; inakuwa ni mali ya mnyama – hiyo pumzi – akiwa nayo, lakini inamrudia Mungu anapokufa.

Ni muhimu sana katika kuelewa somo hili kuwa makini kuhusu ukweli wa “asili ya viumbe” mbalimbali, kama ilivyoelezwa katika Mwanzo NA MUNGU kupitia kwa Musa. Tusitiwe hofu na kuacha habari hizi za Mungu kwa nadharia ya kubahatisha ya “mageuzi” ya viumbe – “evolution.” Ni “sayansi” ya kusikia tu ambayo haijathibitishwa: kila mara ikipitia mageuzi na isiyo imara. Wanadamu wanapozidi kupekua zaidi na kugundua mambo ya nje ili kufahamu zaidi juu ya viumbe wote – ushahidi ulitangazwa kutoka katika hekima na nguvu na ubunifu na kusudi – hesabu ikipigwa mara milioni na zaidi haiwezi kuwa ni matokeo ya kazi isiyo makini ya kubahatisha kama ya mtu asiye na uwezo wa kuona – yaonyesha kabisa ilivyo hii nadharia ya mageuzi kuwa na upungufu mkubwa na ni ovyo.

Nadharia ya mageuzi inampa mwanadamu sababu rahisi ya kumfanya aepukwe na mamlaka ya Mungu na kutii amri zake ambazo zinasulubisha mwili. Jinsi gani mtu na akili zake timamu, na waume kwa wake waamini yale ambayo katika hali nyingine wangeliona kama jambo lisilowezekana kabisa? Mwanadamu kila mara amekuwa na ndoto za ajabu, na kuwa mwepesi wa kuyaamini yote yanayoweza kumnasua na uwajibikaji kwa mkuu kuliko yeye. Mtu asiye na

akili anaweza kuona sura milioni za Mungu kila mahali katika kazi ya uumbaji wa vitu vikubwa na vidogo. Ni imani iliyoje kuamini kuwa uzuri huu wote na hekima na nguvu vimetokea pasipo akili na kusudi, na papo kwa hapo, hivi hivi tu. Upumbavu kama huu wawezaje kuitwa "sayansi?"

Tukimkubali Kristo, na yale aliyosema kama maneno yaliyotokea moja kwa moja kutoka kwa Mungu kupitia kwake (Yohana 14:24), basi itatulazimu kuviamini vitabu vya Musa kwani Kristo alimwidhinisha Musa, na alikubali maelezo yake kuwa ni ya kweli na yaliongozwa na Mungu. Angalia kwa makini maneno haya ya Yesu :-

Musa "aliandika habari zangu: msipoyaamini maandiko yake, mtayaamini wapi maneno yangu?" (Yohana 5: 46 - 47).

Kauli imekamilika. Na agano Jipya yawafunganisha Adamu na Kristo pamoja kama nguzo mbili katika mpango wa Mungu. Wanasimama na kuanguka pamoja kama uhalisia wa kihistoria.

Kwa hivyo twawaona Adamu na Hawa kama watunzaji wa Bustani maridadi ya Edeni, wakawa wanaishi katika hali iliyosemekana kama "NJEMA SANA" (Mwanzo 1:31). Waliwekwa chini ya amri iliyowahitaji wawe watiifu wanaotii na wanaopenda mahitaji ya Mungu. Hali hii ilitawala kwa kusudi ya kuonyesha ya kuwa hii ndiyo ilikuwa njia ya pekee ya kuzalisha raha ya milele kwa mwanadamu, na kupata radhi ya utukufu wa Mungu.

Adamu alikatazwa asile kutoka kwa Mti wa ujuzi wa Mema na Mabaya –

"Walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika" (Mwanzo 2:17).

Hii ndiyo ilikuwa namna rahisi ya kufundisha na kumfunza anavyostahili kukaa na kujihusisha na Mungu. Muda aliokuwa mtiifu kwa Mungu hatujui, lakini twaambiwa wakati fulani, Adamu alimwasi (Mwanzo 3:6) –

"Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala."

Matokeo ya uasi huu ulishughulikiwa kama Mungu alivyokuwa ametangaza awali –

"Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema,Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako… kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana U mavumbi WEWE, nawe mavumbini utarudi."(Mwanzo 3:17 - 19)

Adamu, aliyekuwa na nafasi nzuri ya kupata uzima wa milele, sasa akapata pigo la kurudia hali yake ya kukosa kabisa:- utupu; hali ambayo kwa kurithishwa maumbile ya mwili imewafikia wana wote wa Adamu. Sisi sote tuna miili ya kuharibika, inayokufa, kwa kanuni hii:

“Kutoa kitu kilicho safi kutoka katika kitu kichafu? Hapana awezaye (Ayubu 14:4)”

Sisi sote ni wa kufa, viumbe vya kufa. Baada ya uasi wa Adamu na Hawa, na kuhukumiwa kwao, walifukuzwa kutoka katika Bustani ya Edeni, na wakanyimwa ruhusa ya kuufikilia Mti wa Uzima, kwa sababu hii:

“Asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele; kwa hiyo BWANA Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa” (Mwanzo 3:22 - 23)

Vizazi vya Adamu, wasiohesabika kwa wingi, ni wenye dhambi na maskini, wanatupiliwa mbali kwa rehema, kizazi baada ya kizazi, kama nyasi inavyokatwa.

Kumbuka, ujumbe wa Biblia, unaofuata mantiki fulani. Hapa twaweza kujiuliza sababu ya kukatazwa kuufikia mti wa Uzima, kama tayari walikuwa “Immortal” – na miili ya kudumu, isiyopatikana na mauti – kama walikuwa ni “immortal souls” – “roho zisizoweza kufa,” tayari wamepangiwa “Kuishi milele,” mbinguni au kuzimu. Ikiwa nadharia hii ni kweli, suala la wao kuishi milele au la halingetoka kamwe; ingekuwa ni jambo la kutaka kujua ni kwa hali na namna gani wangeishi maisha yao ya milele. Kule kula – au kutokula matunda ya mti wa uzima ungechangia vipi hali hiyo?

Biblia inatupa maelezo ya kweli, rahisi na ya kimantiki kuhusiana na hali yake ya sasa ya kufa. Na pia ni kutoka kwa kitabu hiki ndipo hatima yake ya siku za usoni zapatikana. Ayubu aliuliza:

“Mtu akifa, je ! Atakuwa HAI TENA?” (Ayubu 14:14)

Biblia pekee ndiyo inayoweza kujibu hili swali. Mbegu ikipandwa ardhini “hufa”, inamea tena; hizo nguvu za kuota zimo katika mbegu. Au mti ukikatwa huchipuka tena, Kama Ayubu anavyosema (vifungu 7 - 9).

Sivyo ilivyo na mwanadamu, mambo huwa kinyume (k 10).

“Lakini mwanadamu hufa,huifariki dunia; Naam, mwanadamu hutoa roho (gava: muda wake huisha) naye yupo wapi?

Hayupo Amerudi katika mavumbi ya ardhi, kuchangamana na mavumbi yote. Kama ataishi tena, itakuwa ni juhudi yake Mwenyezi Mungu.

Matumaini ya watu kuishi tena kwa namna fulani ni habari njema ya ujumbe wa Biblia (1 Wakorintho 15:21).

“Maana kwa kuwa mauti ililetwa na mtu, kadhalika na kinyama ya wafu ililetwa na mtu.”

Kristo alitangaza kuwa yeye ni ufufuo na uzima, akaongezea –

“Yeye aniaminiaye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi” (Yohana 11:25).

Paulo alisema, Kristo atakaporudi duniani, ndiye:

“Atakayeubadili mwili wetu wa unyonge (tapeinosi, Kiyunani - chini) upate kufanana na MWILI wake wa utukufu” (Wafilipi 3:21)

Alimwandikia Timotheo kusema:

“Kristo Yesu, aliyebatili mauti (kama hatima ya wale wanaomtii Mungu) kuufunua uzima na kutoharibika, kwa ile injili.” (2 Timotheo 1:10).

Vifungu vifuatavyo vyafunza mambo sampuli hiyo (angalia kuwa maelezo haya hayana maana kama mtu tayari ana hali ya uzima wa milele ndani yake):

“Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele” (Yohana 10:10)

“Kondoo wangu waisikia sauti yangu … Nami nawapa uzima wa milele” (Yohana 10:28)

“Mungu … akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yohana 3:16)

“Kupotea” ndiyo kinyume cha kupata karama ya uzima wa milele. Juu ya maana ya “kupotea”, Paulo anatumia maneno sawia, akisema kuwa ikiwa Kristo hangefufuka, wale ambao wamelala mauti katika Kristo wangekuwa “wamepotea” (1 Wakorintho 15:18) –

Bila shaka sio kwenda kwa adhabu ya kuteswa milele, na kama neno linavyosema tu ni “kupotea” kwenda na kuwa si kitu, kutoweka. Angalia neno “kupotea” (Kiyunani : appolumi) katika kamusi ya Kiebrania ya Strong – Strong’s Hebrew Dictionary . Dhana ya neno hilo kumaanisha “moto wa milele” au “adhabu ya milele” ingekuwa ni jambo ovyo kabisa popote pale.

Tukikubali nadharia ya “immortal soul” – “roho inayodumu milele” ndilo ambalo tutalazimika kuamini: “Kifo” haimaanishi kifo, lakini ni maisha yasiyopendeza; “Kupotea” sio kupotea; “kuangamia sio kuangamia.”

Kutokana na vifungu vilivyo hapo juu, mafundisho ya Biblia ni bayana: uzima wa milele si kitu alichonacho kila mwanadamu bali ni karama ya Mungu kwa wachache watakaopewa ikiwa watatenda mapenzi ya kusudi lake. Vifungu hivi vyote na zaidi, vyaonyesha ya kuwa uzima wa milele au “immortality” – hali ya kutokufa kabisa, ni kitu cha kutafutwa kwa bidii, karama, kitu ambacho watapewa, “wale ambao kwa saburi katika kutenda mema WANATAFUTA kutoharibika, watapewa uzima wa milele” (Warumi 2:7)

MASWALI

1. Nguvu za kuleta uhai zatoka wapi?
2. Kifo cha mwanadamu na mnyama kinafanana vipi?
3. Ni kitabu kipi kinachotupa maelezo mwafaka kuhusu “asili ya viumbe mbalimbali?”
4. Tukimkubali Kristo, kwa nini yafaa pia kukubali maelezo ya Biblia kuhusu uumbaji?
5. Ni maneno yapi yanaelezea hali ya mwili wa Adamu ulivyokuwa kabla ya kutenda dhambi?
6. Tukio lipi lilisababisha Adamu kuwa na mwili wa kufa?
7. Ni kwa jinsi gani hukumu ya Adamu iliwapata wanadamu wote? Andiko gani lathibitisha hili?
8. Twajuaje kuwa Adamu hakuwa na mwili wa kutokufa?
9. Je, mwanadamu huibuka akawa hai tena akisha kufa?
10. Ni kupitia kwa mtu gani suala la ufufuo lawezekana?
11. Ni watu wa nasaba gani watakaopata uzima wa milele?